# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS – TAMISEMI
# HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

NAMBA ZA SIMU 0766480580/0621-050499
Mkuu wa Shule:
Makamu Mkuu wa Shule: 0759-375334
UNAPO JIBU TAFADHALI TAJA
Kumb. Na. MZY/SS/J/A/VOL 6/06

SHULE YA SEKONDARI MWAZYE
S. L. P 02
MATAI – KALAMBO.
………/……. /2022.

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI
……………………………………………….
S. L. P …………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKASHULE YA SEKONDARI MWAZYE HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO MKOA WA RUKWA MWAKA 2022/2023.**

Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule ya sekondari Mwazye kwa mwaka 2022. Kwa tahasusi ya ………………………………….

Shule ya Sekondari Mwazye ipo umbali wa km 60 mwa mji mkuu wa mkoa wa Rukwa (Sumbawanga mjini). Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga unapatikana katika kituo cha mabasi cha Sumbawanga kwa nauli ya Tsh 4,000/=

Muhula wa masomo unaanza tarehe ....../......2022 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe ...../...../2022 na mwisho wa kuripoti ni tarehe ....../...../2022.

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. SARE YA SHULE

I. WAVULANA

- Anatakiwa awe na Suruali mbili (02) yaani Nyeusi na Brown (Rangi ya vitambaa imeambatanishwa).
  Mshono wa suruali: Iwe mifuko mitatu mmoja nyuma upande wa kulia na miwili pande zote kulia na kushoto pembeni na siyo ya kubandika, iwe na rinda mbili kila upande na upindo wa chini (miguuni) ugeuzwe juu (turn up) upana miguuni uwe wa kutosha isiwe ya kubana.
  NB: Suruali za mitumba na jeans haziruhusiwi hapa shuleni
- Mashati mawili (02) meupe yenye mikono mirefu (Long sleeves)
- Viatu vyeusi jozi mbili (2) vya ngozi vya kufunga na kamba visiwe na soli ndefu na visivyochongoka mbele.
- Soksi jozi mbili (2) rangi nyeusi
- Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi
- Sweta la Bluu yenye shingo “V” kwa ajili ya kujikinga na baridi
- Tai mbili yaani nyeusi na Brown

II. WASICHANA

- Anatakiwa awe na Sketi mbili (02) yaani nyeusi na Brown vitambaa vinapatikana shuleni
  Mshono wa sketi: Ziwe na marinda kumi na mbili (12). NB: Sketi zote ziwe ndefu zifike kwenye viatu, sketi fupi hazihitajiki.
- Mashati mawili (02) meupe mikono mirefu (long sleeves)
- Viatu vyeusi jozi mbili (02) vya ngozi vya kufunga na kamba, visiwe na soli ndefu na visivyochongoka mbele.
- Soksi jozi mbili (2) rangi nyeupe
- Sweta la Bluu yenye shingo "V" yenye nembo ya shule kwa ajili ya kujikinga na baridi inapatikana sheleni kwa gharama ya Tshs. 13,500/= ( elfu kumi na tatu mia tano tu).
- Tai mbili yaani nyeusi na Brown
- Rangi ya hijab ifanane na sare ya shule (nyeupe).
- Awe na shamba dress rangi ya damu ya mzee draft kwa ajili ya kushindia.
- Nywele ziwe fupi muda wote, hakuna kusuka nywele wala kuweka dawa.

  NB: Kiambata kwa ajili ya sare za shule kinapatikana nyuma ya fomu hii.

B. SARE YA MICHEZO

I. WAVULANA

- Awe na Bukta au tracksuit rangi ya blue bahari
- T-shirt rangi ya damu ya mzee
- Raba jozi 01 kwa ajili ya michezo

II. WASICHANA

- Awe na tracksuit rangi ya blue bahari
- T-shirt rangi ya damu ya mzee
- Raba jozi 01 kwa ajili ya michezo

C. ADA NA MICHANGO YA SHULE

(a) ADA

- Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/= kwa mwanafunzi unaweza kulipa kiasi cha Tshs 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule yenye jina la akaunti MWAZYE SECONDARY SCHOOL (62101100049) katika benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).

(b) MICHANGO MINGINE INAYOTAKIWA KULIPWA NA KILA MZAZI NI

- Tshs 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
- Tshs 6,000/- kwa ajili ya kitambulisho na picha
- Tshs 20,000/= kwa ajili ya Taaluma
- Tshs 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine
- Tshs 2,000/= kwa ajili ya nembo ya shule
- Tshs 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza (Tshs 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya Tshs 5,000/=)

- Tshs 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (haitarejeshwa)

NB: Michango yote katika kipengele B iingizwe kwenye akaunti yenye jina SHULE YA SEKONDARI MWAZYE (62110001827).
(Tafadhari andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).
NB: Mwanafunzi ahakikishe anakamilisha michango yote endapo atakuwa hajakamilisha hatapokelewa.

(c) ADA YA MITIHANI

- Mtihani wa Taifa (ACSEE)
- Mitihani ya kujipima (Mock examinations)
- Pre-National examinations
- Mitihani ya joint mkoa kwa kidato cha tano

NB: Michango ya mitihani ni kwa kidato cha sita isipokuwa joint examinations
NB: Fedha kwa ajili ya ziara za masomo (study tour) italipwa wakati wa ziara.

(d) MAHITAJI MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KULETA SHULENI

(i) Ream ya karatasi 01 (A4)
(ii) Vitabu vya masomo ya General Studies, History, Geography, English language na Kiswahili
(iii) Godoro 01 Ft 2 ½ x 6
(iv) Tranker 01 (Sanduku)
(v) Mashuka ya blue na pink pair 02, Blanketi 01, Foronya 01, Chandarua 01
(vi) Vyombo vya chakula. Sahani 01, Bakuli 01, Kijiko 01 na Kikombe 01
(vii) Ndoo mbili ndogo zenye mifuniko
(viii) Kwanja 01, Jembe 01, Reki 01, ufagio wa ndani (soft broom) 01,wa nje (chelewa) 01 na Squeezer ( kikaushio cha maji) 01.
(ix) Kiti na Meza.

(e) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu yenye dhamana nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule
(c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation)
(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii

(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
(g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Vitu kama bangili, hereni, pete, kofia n.k haviruhusiwi kuvaliwa shuleni. Ukikutwa navyo utanyang'anywa na vitachomwa moto na adhabu nyingine itafuata.

(f) MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
3. Kugoma, kuhamasisha/kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla
5. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule
6. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika au kuweka dawa nywele (wanafunzi wote watatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni)
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya
9. Uvutaji wa sigara
10. Uasherati, uhusiano wa jinsia moja (ushoga)
11. Kupata mimba au kutoa mimba
12. Ubakaji
13. Kushiriki katika matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
14. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
15. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni
16. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
17. Kudharau bendera ya Taifa
18. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
19. Kukataa adhabu kwa makusudi
20. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

(g) VIAMBATISHO NA FOMU MUHIMU

i. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospital ya serikali
ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai
iii. Mzazi/mlezi unatakiwa kujaza Fomu ya kukiri kukubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada na michango mingine na maelekezo yote yatakayotolewa na shule
iv. Unatakiwa kuja na Picha nne (04) za wazazi na ndugu wa karibu watakaoweza kukutembelea shuleni pamoja na namba zao za simu
v. Unatakiwa kuja na cheti cha kuzaliwa (nakala) au affidavit of birth

NB: Viambatisho na fomu hizo akabidhiwe makamu mkuu wa shule wakati wa kuripoti

Tafadhali soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SHULE YA SEKONDARI MWAZYE

……………………..
JANETH M. AKO
MKUU WA SHULE

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KALAMBO DISTRICT COUNCIL

MWAZYE SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 03,
MATAI-KALAMBO.
DATE:……………………

MEDICAL OFFICER,
GOVERNMENT HOSPITAL,
P.O.BOX………………

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATIONS

Please examine……………………………............. as to his/her fitness for pursuing further.

1. Hemoglobin
2. P.V. Bleeding
3. Blood pressure (BP)
4. Blood group
5. Sight
6. Hearing
7. Urine for pregnancy test (UPT)
8. Stool for routine examination
9. Asthma
10. Skin diseases
11. Leprosy
12. Epilepsy
13. Pulmonary tuberculosis
14. Deformity
15. Mental problems
16. V.D. (GVE TYPE)
17. MRDT
18. Any other serious diseases (not mentioned above)……………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………

| COMMENTS | DESIGNATION AND SIGNATURE |
|---|---|
| …………………………………………… | ………………………………………………………………………… |
| …………………………………………… | ………………………………………………………………………… |
| …………………………………………… | ………………………………………………………………………… |
| ……………………………………………… | ………………………………………………………………………… |

OFISI YA RAIS – TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO
SHELE YA SEKONDARI MWAZYE

# MKATABA

Unashauriwa kujaza fomu hii ya mapatano kikamilifu

## SEHEMU A: MWANAFUNZI

Mimi ………………………………………………………………………. Nimesoma na kuelewa vizuri sheria, maagizo na kanuni zote za shule, nakubali/sikubali nafasi hii na kuwa nitatumia uwezo wangu wote kujiendeleza kitaaluma, nitatii sheria, maagizo na kanuni zote za shule na wala sitashiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.

SAHIHI ……………………………… TAREHE ……………………….

## SEHEMU B: MZAZI/MLEZI

Mimi ……………………………………………………………. Mzazi/mlezi wa ………………………………….. Nimepokea taarifa ya mwanangu ya kujiunga na shule ya sekondari Mwazye. Kwa kutambua umuhimu wa Elimu na wajibu wangu, naahidi kuwa muda wote mwanangu atakapokuwa shuleni nitashirikiana na Uongozi wa shule kumlea mtoto kwa kufuata sheria, maagizo na kanuni zote za shule na kuhakikisha kuwa anahudhuria masomo kwa kadri ya ratiba ya shule, nitatekeleza maelekezo yote yatakayotolewa na shule na nitatoa Ada na michango mingine yote ya shule iliyopitishwa kwa wakati.

SAHIHI ……………………………… TAREHE ………………………….

PICHA ZA SARE ZA SHULE





